DNA (Vinasaba) ni Nini?

DNA Ni kifupi cha neno (Deoxyribonucleic Acid). Hizi ni chembechembe asili za urithi au viini tete ambavyo hupatikana katika kila kiumbe hai.

Msingi wa Uchunguzi wa DNA (Vinasaba)

Kila Binadamu ana mpangilio wa chembechembe asili za urithi aliyorithi kutoka kwa wazazi wote wawili (Baba na Mama). Mpangilio wa chembechembe asili za urithi hurithiwa nusu kutoka kwa baba na nusu kutoka kwa mama.

Hivyo basi ili kutambua uhalali wa mzazi kwa mtoto ni lazima mtoto awe na chembechembe asili za urithi nusu zinazooana na za baba na nusu nyingine zinazooana na za mama.

Mfn.1: UHALALI SAHIHI WA MZAZI KWA MTOTO

UHALALI WA WAZAZI KWA MTOTO.
Asilimia 99.99% ndiye mzazi halali wa kumzaa mtoto.



Mfn.2: UHALALI USIOSAHIHI WA MZAZI KWA MTOTO

UHALALI WA MZAZI (BABA) KWA MTOTO. Asilimia 0.00%. Baba sio mzazi halali wa kumzaa mtoto.



DNA (Vinasaba) Hupatikana wapi?

DNA (Vinasaba) hupatikan katika vielelezo tofauti navyo ni:

- Damu kavu na damu majimaji,
- Majimaji ya kiume,
- Mifupa,
- Unywele wenye mzizi,
- Mate,
- Kucha,
- Vichungi vya sigara,
- Vitu vinavyomilikiwa binafsi kama vile miswaki, nyembe, mavazi, n.k

Umuhimu wa kuwepo kwa Sheria ya kusimamia na kudhibiti matumizi ya DNA (Vinasaba) vya Binadamu:

1 Matumizi ya DNA (Vinasaba)

Matumizi ya Teknolojia ya DNA (Vinasaba) yamepanuka kwa sekta binafsi, hivyo kuhitaji Sheria inayosimamia, kuratibu na kudhibiti utoaji wa huduma ya Tekinolojia hii.

2 Uchukuaji wa sampuli za DNA (Vinasaba) vya Binadamu

DNA (Vinasaba) vya Binadamu hubeba taarifa binafsi za siri za chembechembe asili za urithi au viini tete za kila kiumbe ikiwemo za binadamu, Hivyo kunahitajika usimamizi na udhibiti wa ukusanyaji, uhifadhi, ufungashaji, usafirishaji, upokeaji, uchunguzi, utoaji wa majibu na uteketezwaji wa Sampuli za DNA ya Binadamu unaozingatia maadili ya kitaalamu na miongozo ya Kisheria ili kuweza kuzuia madhara yanayo weza kujitokeza kutokana na matumizi mabaya ya teknolojia hii.

3. Uchunguzi wa vielelezo vinavyo husishwa na Upelelezi wa Makosa ya Jinai

Matokeo ya uchunguzi wa DNA (Vinasaba) utasaidia kuondoa mapungufu yatakayojitokeza katika upelelezi wa Makosa ya Jinai na hivyo kurahisisha utoaji wa haki katika vyombo vya kisheria.

4. Uchunguzi wa vielelezo vinavyo husishwa na Migogoro ya kijamii (Civil Cases)

Mchakato mzima wa uchunguzi wa DNA (Vinasaba) mpaka upatikanaji wa matokeo ya uchunguzi.

Mchakato wa uchunguzi wa DNA (Vinasaba) huchukua wiki mbili hadi nne. Aidha, inaweza ikachukua muda mrefu kutegemeana na aina ya sampuli na taratibu zake za uchunguzi, umahiri wa sampuli ikiwa imeharibika sana au ya zamani.

5 Sheria ya Usimamizi wa Vinasaba vya binadamu Sura ya 73

- Inaainisha taratibu mbalimbali za kufuatwa na kutekelezwa,majukumu ya sekta zinazohusika katika utekelezaji wa sheria hii,
- Inaweka utaratibu wa kuzingatia katika kufanya tafiti mbalimbali za magonjwa , dawa na lishe,
- Inaweka wazi haki za mtu anayetoa sampuli za DNA ya Binadamu,
- Inaonyesha utaratibu wa utoaji fidia kwa mtu anayeathirika na ukiukwaji wa haki zake chini ya sheria hii,
- Inaonyesha utaratibu wa kuweka siri za matokeo na kuweka mipaka ya matumizi ya sampuli za DNA (Vinasaba) ya Binadamu. Aidha, inaainisha makosa na adhabu zake kwa maabara, taasisi, asasi na watu watakaokiuka utaratibu mzima wa matumizi ya Teknolojia hii ya Uchunguzi wa sampuli za DNA ya Binadamu.

Kwa maelezo zaidi wasiliana na:

Mkemia Mkuu wa Serikali
Wakala wa Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali
Luthuli/ Barack Obama Drive
S.L.P. 164
Dar Es Salaam, Tanzania
Simu: + 255 22 2113383/4
Nukushi: +255 22 2113320
Baruapepe: cgc@gcla.go.tz, gcla@gcla.go.tz

Meneja
Maabara ya Kanda ya Mashariki
Luthuli/Barack Obama Drive
S.L.P. 164
Dar Es Salaam, Tanzania
Simu: + 255 22 2113383/4
Nukushi: +255 22 2113320
Baruapepe: gcla.east@gcla.go.tz

Meneja
Maabara ya Kanda ya Ziwa,
Eneo la Hospitali ya Sekou Toure/Isamilo
S.L.P. 502,
Mwanza, Tanzania.
Simu: +255 28 2500279
Baruapepe: gcla.lake@gcla.go.tz

Meneja
Maabara ya Kanda ya Kaskazini
Kituo cha Afya Themi
S.L.P. 2095
Arusha, Tanzania.
Simu: +255 27 2506394
Nukushi: +255 27 2549026
Baruapepe: gcla.north@gcla.go.tz

Meneja
Maabara ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini
Eneo la Hospitali ya Mkoa wa Mbeya
New Forest Area
S.L.P. 2875
Mbeya ,Tanzania.
Simu: +255 25 2502311
Nukushi: +25525 250 312
Barua pepe: gcla.southern@gcla.go.tz

Meneja
Maabara ya Kanda ya Kusini
Ushirika House
Barabara ya TANU
S.L.P. 1414
Mtwara,Tanzania.
Simu: +255 23 233 4760
Nukushi: +255 23 233 4761
Barua pepe: gcla.south@gcla.go.tz

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO

WAKALA WA MAABARA YA MKEMIA MKUU WA SERIKALI

ISO 9001:2008
ISO 17025:2005

IDARA YA SAYANSI JINAI NA HUDUMA ZA VINASABA

SHERIA NA TEKNOLOJIA YA UCHUNGUZI WA VINASABA (DNA) VYA BINADAMU